




Kuja Norwei

Å komme til Norge

-  Aamiina
-  Julie Cornelia van Walsum
-  Jacob Haule
-  5
-  Kiswahili sw / norsk nb



Mimi na kaka zangu wawili tulikuja Norwei mwezi Disemba 2016. Tulivaa nguo za majira ya joto kwa sababu tulifikiri Norwei kutakuwa na joto kama Somalia. Hata hivyo, tulipofika uwanja wa ndege kulikuwa na theluji. Tulihihi baridi na hali ya hewa ilikuwa ya baridi sana. Ingawa tulibeba mabegi, yalikuwa na nguo za majira ya joto tu.

. . .


De to brødrene mine og jeg kom til Norge i desember 2016. Vi hadde på oss sommerklær fordi vi trodde det ville være like varmt i Norge som i Somalia. Men da vi kom til flyplassen, snødde det. Vi frøs og været var kaldt. Selv om vi hadde med oss noen koffert, inneholdt de bare sommerklær.



Hata kama kulikuwa na baridi, nilifurahi sana tulipokuja Norwei. Hatimaye niliweza kufanikiwa kuonana tena na mama yangu ambaye sikumuona kwa miaka sita. Tulionana na mama pamoja na rafiki zake wawili. Tulipomuona tulilia kwa furaha. Tulienda kwenye mji mdogo ambapo mama anaishi.

. . .

Selv om det var kaldt, var jeg veldig glad da vi kom til Norge. Jeg kunne endelig møte mamma igjen, som jeg ikke hadde sett på seks år. Mamma og to av venninnene hennes møtte oss. Da vi møtte mamma igjen, gråt vi av glede. Mamma bor i en liten by, så vi kjørte dit.



Siku za mwanzo tukiwa katika mji wa mama zilikuwa ni za kustaajabisha. Kulikuwa na baridi na theluji na hatukuweza kuona chochote. Mitaa ilikuwa tupu kabisa. Watu wachache niliokutana nao walionekana wakihihi baridi na hawakuwa sawa. Somalia kulikuwa na watu kila mahali, kwa hiyo kila kitu kilikuwa kigeni hapa. Mama yangu na rafiki zake walitupatia zawadi na kisha akatupeleka kununua nguo za majira ya baridi.

. . .

De første dagene i mammas by var veldig merkelige. Det var kaldt, det snødde og det var lite å se. Gatene var helt folketomme. De få personene jeg møtte, virket kalde og uvennlige. I Somalia er det folk overalt, så alt føltes uvant her. Mammaen min og venninnene hennes ga oss gaver, og hun tok oss med for å kjøpe vinterklær.

Baada ya mapumziko ya Krismasi, nilijiunga na kozi ya Kinorwei katika kituo cha elimu ya watu wazima. Nilisoma pale kwa muda wa miaka miwili kabla ya kuanza shule ya msingi. Sasa nipo mwaka wa mwisho na nimejitengenezea marafiki wengi. Ninapenda sana kuongea na watu na kufurahia kuonana na watu wapya.

. . .

Etter juleferien begynte jeg på norskkurs på voksenopplæringscenteret. Jeg gikk der i to år før jeg begynte på en vanlig skole. Nå går jeg siste året, og jeg har fått mange nye venner. Jeg er veldig sosial og jeg er glad i å møte andre.



Baada ya masomo, huwa ninaenda kwenye kituo kinachoendeshwa na wajitoleaji ambapo huwa ninasaidiwa kufanya kazi ya nyumbani. Pia nimejiunga na kozi ya kushona katika kituo hiki.

. . .

Etter skolen drar jeg til Frivilligsentralen for å få hjelp med leksene. Jeg har også begynt på et sykurs der.



Nilipokuwa Somalia, sikuwahi kwenda shule au kujiunga na kozi yoyote isipokuwa shule ya Kuran. Sikujua kusoma wala kuandika. Sasa nimeshajifunza namna ya kuandika Kisomali na Kinorwei na masomo mengine mengi. Bila elimu, nilijihisi si kitu. Sasa ninajiona mwenye maarifa na furaha.

. . .

I Somalia fikk jeg aldri mulighet til å gå på skole eller ta et kurs, bortsett fra koranskole. Jeg kunne ikke lese eller skrive. Nå har jeg lært å skrive på både somali og norsk, og mange andre fag. Uten utdanning følte jeg at jeg ikke var noen. Nå føler jeg meg kunnskapsrik og glad.



Mwaka ujao, nitaanza shule ya sekondari katika idara ya afya na maendeleo ya vijana. Hapo baadaye, ninataka kuwatumikia vijana. Nikimaliza elimu yangu, ndoto yangu ni kupata ajira ya kudumu. Pia ninataka kujifunza udereva na nipate leseni yangu ya udereva.

. . .

Neste år skal jeg begynne på helse- og oppvekstfag på videregående skole. I framtiden vil jeg bli barne- og ungdomsarbeider. Når jeg er ferdig med utdanningen min, drømmer jeg om å få meg en fast jobb. Jeg vil også lære å kjøre bil og ta førerkort.



Kama ngingebaki Somalia, ninadhani ningekuwa mama mpaka sasa. Pengine ningekuwa na watoto wengi. Kama ningekuwa Somalia, nisingekuwa na fursa sawa kama nilizozipata mpaka sasa. Ninajihisi mwenye bahati kuishi Norwei.

. . .

Hvis jeg fremdeles hadde bodd i Somalia, hadde jeg kanskje vært mor nå. Kanskje jeg hadde fått mange barn allerede. Hvis jeg hadde vært i Somalia, ville jeg ikke hatt de samme mulighetene som jeg har fått nå. Jeg føler meg heldig som bor i Norge.



LIDA Stories

lidastories.net

Kuja Norwei

Å komme til Norge

 Aamiina

 Julie Cornelia van Walsum

 Jacob Haule (sw), Espen Stranger-Johannessen (nb)

